

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA TATU

YATOKANAYO NA KIKAO CHA AROBAINI NA TISA

23 JUNI, 2016

MKUTANO WA - TATUYATOKANAYO NA KIKAO CHA AROBAINI NA NANE

TAREHE 23 JUNI, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

Makatibu Mezani:

1. Dkt. Thomas Kasilillah
2. Ndg. John Joel
3. Zainab Issa
4. Lawrence Makingi

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

Waheshimiwa Wabunge wafuatao walipata nafasi kumuuliza maswali Mhe. Waziri Mkuu:-

- | | | |
|-------------------------------------|---|-----|
| 1. Mhe. Venance Methusallah Mwamoto | - | CCM |
| 2. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah | - | CCM |
| 3. Mhe. Richard Philip Mbogo | - | CCM |
| 4. Mhe. Cosato David Chumi | - | CCM |
| 5. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa | - | CCM |

III. MASWALI YA KAWAIDA:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge:-

OFISI YA WAZIRI MKUU:

Swali Na.419 – Mhe. Omar Mohammed Kigua
Swali la nyongeza: Mhe. Omar Mohammed Kigua

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na.420 Mhe. Amina Saleh Mollel [kny. Dkt Elly Marco Macha]
Swali la nyongeza: Mhe. Amina Saleh Mollel

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na.421 – Mhe. Sixtus Raphael Mapunda
Swali la nyongeza: Mhe. Sixtus Raphael Mapunda

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Swali Na.422 – Mhe. Josephine Genzabuke [kny. Neema William Mgaya]
Swali la nyongeza: Mhe. Josephine Genzabuke

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Swali Na.423 – Mhe. Faida Mohammed Bakar [kny. Khatib Said Haji]

Swali la nyongeza: Mhe. Faida Mohammed Bakar

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

Miswada ya Sheria ya Serikali ifuatayo ilisomwa kwa mara ya kwanza:-

- i) Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari wa mwaka 2016 (*The Access to Information Bill, 2016*).
- ii) Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa Mwaka 2016 (*The Valuation and Valuers Registration Bill, 2016*).
- iii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016 (*The Government Chemist laboratory Authority Bill, 2016*).
- iv) Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016 (*The Chemist Professionals Bill, 2016*).

V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

1. Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2016 (*The Finance Bill, 2016*) ulisomwa kwa mara ya pili. Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Philip Mpango aliwasilisha maelezo ya Muswada huu wa Sheria.
2. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti aliwasilisha Taarifa ya kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2016 (*The Finance Bill, 2016*).

MATANGAZO

Kabla Naibu Spika hajamwita mwakilishi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuwasilisha taarifa yao aliwatangaza wageni mbalimbali walioko kwenye “galleries” za ukumbi wa Bunge.

MWONGOZO WA SPIKA

Mhe. Kemilembe Julius Lwota aliomba mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na kuomba Naibu Spika atoe muda kwa Waheshimiwa Wabunge kuupitia Muswada wa Sheria ya Fedha uliotolewa tena ambao umefanyiwa marekebisho kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Spika alikubaliana na hoja ya Mhe. Kemilembe na kwamba atatoa muda huo ila Wabunge wakubali kuwa namba ya wachangiaji itapungua, hivyo aliwahoji Wabunge na walikubali uamuzi huo wa kiti.

VI. KUSITISHA BUNGE:

Baada ya Wabunge kukubali uamuzi huo, Naibu Spika alisitisha shughuli za Bunge saa 5:30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni ili Waheshimiwa wapate nafasi ya kuusoma Muswada huo wa Fedha uliochapishwa tena.

VII. BUNGE KUREJEA:

Shughuli za Bunge zilirejea saa 10.00 jioni na Naibu Spika aliongoza kikao. Majadiliano yaliendelea kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka, 2016 (*The Finance Bill, 2016*) ambapo Waheshimiwa Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchangia:-

- | | | |
|--------------------------------------|---|-----|
| 1) Mhe. Abdallah Hamis Ulega | - | CCM |
| 2) Mhe. Ally Mohamed Keissy | - | CCM |
| 3) Mhe. Joseph George Kakunda | - | CCM |
| 4) Mhe. John Constantino kanyaswi | - | CCM |
| 5) Mhe. Jitu Vrajlal Soni | - | CCM |
| 6) Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma | - | CCM |
| 7) Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi | - | CCM |
| 8) Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo | - | CCM |

Mheshimiwa Spika alimwita mtoa hoja kuhitimisha hoja yake.

VIII. KAMATI YA MATUMIZI

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi kupitia Muswada Kifungu kwa Kifungu. Pamoja na baadhi ya Wabunge kuomba ufafanuzi kwenye Vifungu vya Muswada, Bunge lilipitisha Muswada huu.

IX. BUNGE KURUDIA

Baada ya Bunge kurudia mtoa hoja alitoa taarifa ya shughuli za Kamati ya Matumizi na Naibu Spika alihoji Bunge na kupitisha Muswada wa Fedha wa Mwaka 2016 na kusoma mara ya tatu.

X. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 12.40 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka tarehe 24/6/2016 saa tatu Asubuhi.

**DODOMA
23 JUNI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**